

## **Mtazamo wa Kijumla kuhusu Ushairi wa Kiswahili nchini Kenya: Mifano kutoka Pwani na Bara**

*Rayya Timammy<sup>1</sup> na Mosol Kandagor<sup>2</sup>*

<sup>1</sup>*Chuo Kikuu cha Nairobi*

<sup>2</sup>*Chuo cha Moi*

### **Ikisiri**

Kwa karne nyingi, ushairi umekuwa umekita mizizi katika sehemu za pwani ya Kenya hasa maeneo ya Lamu. Ushairi huu ulifika mpaka sehemu za bara, mahali ambapo Kiswahili kilitumika kusambazia biashara na dini. Hata hivyo, bado hakukuwa na kazi za ushairi za watu wa bara hadi miaka ya kukaribia kipindi cha uhuru katika sehemu za Afrika Mashariki. Japo Kiswahili sasa kinatumika kote nchini Kenya, katika makala hii tuaangalia washairi wa kutoka maeneo haya mawili. Aidha, tutabainisha sifa zinazobainisha ushairi huu wa sehemu hizi mbili; yaani unavyofanana na kutofautiana katika sifa zake za kimaudhui na kimtindo. Vilevile, tutaangalia tofauti za watanzi, lugha wanayoitumia na maswala yanayowashughulisha katika ushairi huu. Mbinu kubwa tuliyotumia ni utafiti wa maktabani uliotuwezesha kupata vitabu na rekodi nyingine. Matokeo muhimu yanabainisha kuwa, washairi wa pwani, hawawezi kuepuka athari ya dini ya Kiislamu katika utunzi wao. Pia, tulibaini kwamba, washairi wa pwani walitumia lahaja zao. Swala lingine muhimu tulilolibaini ni kuwa, washairi wa kike ni wachache sana na hata idadi ya machapisho yao yanapatikana kwa uchache sana nchini Kenya.

**Maneno Muhimu:** Ushairi, Kenya, Kiswahili, Pwani, Bara, Maudhui, Mtindo.

### **Utangulizi**

Ushairi umekuwa ukitumika kwa muda mrefu sana katika maeneo ya pwani. Historia ya ushairi wa Kiswahili ni kongwe kama ilivyo fasihi simulizi na historia ya jamii ya Waswahili. Hii ni kwa sababu ushairi wa awali wa Waswahili ulikuwa ushairi simulizi kabla ya majilio ya wageni wa Kiarabu na hati za Kiarabu katika kuandikia ushairi. Huu ulikuwa ushairi uliotungwa katika miktadha maalumu na ushairi mapokezi uliooghaniwa na kuimbwa katika shughuli za kijamii. Hizi ni zile nyimbo zilizokuwa zikiimbwa katika shughuli, matukio na sherehe mbalimbali kama nyimbo za gungu na lelemama au ushairi uliohusishwa na ufanyaji kazi kama vave na kimai (Pate). Ushairi huu wa fasihi simulizi ulihuushwa pia na utendaji kwa sababu uliwasilishwa kwa hadhira kwa kutegemea sauti, kwa kuimbwa au kughaniwa. Tungo hizi ziliambatanishwa na ala za muziki, mapigo ya ngoma, kupigwa kwa makofi pamoja na sifa nyinginezo zinazohusishwa na utendaji kama kubadilishwa kwa sauti, ishara za uso na kadhalika. Sababu hizi ndizo hasa ziliufanya ushairi huu kujulikana kama ushairi simulizi.

Kezilahabi (1973), Knappert (1979), Senkoro (1988), Njogu na Chimerah (1999), King'ei na Kemoli (2001) na Shitemi (2010) wanakubaliana kuwa ushairi andishi wa Kiswahili unaweza kugawanywa katika awamu nne. Awamu hizo ni kipindi cha urasimi mkongwe, kipindi cha utasa, kipindi cha urasimi mpya na kipindi mambo leo au cha sasa. Kwa hakika tunajua kuwa, ushairi wa Kiswahili ulikuwa unatumiwa pwani pekee katika vipindi vyta urasimi mkongwe, utasa na urasimi mpya. Pengine nchi ya Tanzania ilitumia ushairi katika kipindi cha urasimi mpya lakini katika nchi ya Kenya tunaweza kusema kuwa ushairi ultumika bara kutokea kipindi cha mambo leo au usasa. Kama asemavyo Abedi (1954:1):

zamani utungaji wa mashairi ya Kiswahili ulikuwa umeenea japo si kama hivi leo, na hasa ni fani ya Waswahili ambao waliyatunga kwa kutumia herufi za Kiarabu.

Kipindi cha urasimi mkongwe ni kipindi kinachoenda sambamba na fasihi simulizi ya Waswahili. Nyingi ya tungo hizi zilihifadhiwa katika kumbukumbu za Waswahili na pia nyingine kuandikwa kwa kutumia hati za Kiarabu. Shitemi (2010:3) anasema kuwa:

kipindi hiki kinatambulisha wakati ambapo ushairi wa Kiswahili ulikuwa ni amali ya jamii na ulikuwa haujaenea kwingineko barani Afrika au Afrika Mashariki bali uliathirika na kutagusana na tamaduni za ushairi wa ugenini, hasa Uarabuni kadri ya mitagusano mingine ya kijamii, kibiashara na kidini baina ya jamii hizi.

Mbali na tungo zile za fasihi simulizi, tungo zilizohifadhiwa za wakati huo ni kama Hamziyya, Utensi wa Tambuka, Inkishafi, MwanaKupona, Mikidadi na Mayasa, Shufaka, mashairi ya Fumo Liyongo, Muyaka na Ali Koti na nyinginezo.

Katika kipindi cha utasa (1890 – 1945), ni kazi au tungo chache zilizopatikana zilizotungwa wakati huu pwani, ijapokuwa nyingi zilikuwa za kipindi cha mapema zilizotafitiwa, zikachanganuliwa na kutafsiriwa kwa Kiingereza na wataalamu wa kigeni kwa usaizidi wa wenyeji. Kazi chache zilizopatikana za kipindi hiki zilikuwa za watunzi kama Muhamad Kijumwa na Mwalimu Sikujua.

Katika kipindi cha urasimi mpya ndipo tunaweza kusema kuwa ushairi kama sanaa ulikuwa umeenea toka sehemu za Kaskazini na kudhihirika katika maeneo ya Kusini mwa Us wahili. Hiki ni kipindi ambacho kulizidi kuibuka washairi wa pwani na maeneo mengine na wakazivumbua upya kunga za utunzi na kuzitumia katika utungaji wao. Kipindi hiki ndicho kinachojulikana kama urasimi mpya. Kipindi cha mambo leo au cha sasa kulingana na Shitemi (2010) kinaanzia 1970. Sasa hapa ndipo tunapopata washairi wa bara wa Kenya kwani ndipo walipoanza kutunga na kazi zao zikaanza kuonekana.

### **Washairi wa Kiume**

Katika sehemu hii tumejadili mitazamo ya kijumla kuhusu washairi wa kiume kutoka pwani na bara nchini Kenya.

### **Washairi wa Kiume kutoka Pwani**

Hawa ni wengi sana katika hizo awamu mbalimbali zilizotajwa za ushairi. Washairi hawa wanapatikana katika sehemu au janibu mbalimbali za Us wahilini katika upwa wa Kenya kuanzia Siu hadi Vanga. Kati ya hawa, kuna wengine ambao kumepatikana kazi zao nyingi za utunzi na kuna wengine ni majina yao tu ambayo pengine yanajulikana au tungo ambazo zinasemekana ni zao na hivyo kunahitajika utafiti mwingi kufanywa. Washairi hao wanaweza kugawanya katika matapo mawili. Kuna wale walioandika tungo za kidini zilizosifika kwa mfano watunzi kama Sayyid Aidarus bin Athman (1749 tafsiri ya Ummul Quraa- Hamziyya), Sayyid Abdalla bin Ali bin Nassir (1720 – 1820 Inkishafi), Bakari Mwengo (1760- 1830) na Abubakar bin Abdurahman au Mwenye Mwansabu (1828- 1922).

Kuna na wale walioandika tungo za maudhui mengine lakini mara nyingi kwa kuwa ni waislamu mara nyingi walichukulia mtazamo wa Kiislamu. Watunzi kama Zahidi Mngumi (1758- 1828) alikuwa mshairi mwanasiasa, Alii Koti (1776- 1834) ambaye alikuwa ni mshairi wa Pate, Muhammad bin Sheikh Mataka (1825- 1868) na Muhamad Kijumwa wakitoka maeneo ya visiwa vya Lamu. Kutoka Mvita tunawapata washairi kama Muyaka wa Muhaji (1776- 1840), Suud bin Said Al – Maamiry (1810- 1878), Muhammad Ahmad Al- Mambasy (1820- 1893), Ayubu Mtwana wa Sumba, Mwalimu Sikujua bin Abdala na Ahmad Basheikh Hussein tukitaja wachache.

Washairi wa karne ya 20 na 21 ni wengi sana. Kuna wale ambao, kwa sababu wakati huo uchapishaji uliwezekana kwa urahisi zaidi, hivyo wapo wale waliokuwa tayari wamechapisha kazi zao. Washairi hawa ni kama Ahmad Nassir Juma Bhalo (1936-2019 *Malenga wa Mvita,Taa ya Umalenga* na *Utenzi wa Mtu ni Utu*), Abdilatif Abdalla (*Sauti ya Dhiki, Utenzi wa Adamu na Hawaa*), Boukhet Amana (*Malenga wa Vumba*), Musa Mzenga (*Utenzi wa Nabii Issa* ) na Said Omar Hijazy (*Tujifunze Mashairi* 1977), Said Karama (*Kusoma na Kufahamu Mashairi Ktb 1 &2 1973&1974, Nyota ya Ushairi* 1985 ), Abdalla Barua, Abdalla Said Kizere, Ahmed Sheikh Nabahany 1927-2017

*Umbuji wa Mnazi, Umbuji wa Kiwandeo, Sambo ya Kiwandeo*), Ali Abdullah Ali El – Maawy (*Jawabu ya MwanaKupona*), Hassan Mwalimu Mbega (1914), *Upisho wa Umalenga* (1973), *Dafina ya Umalenga* (1984), *Utenzi wa Mfalme Muadilifu* (1985) ). Mwinyi Matano, Twalib Ali Salim Basaidah (*Bustani ya Mashairi* 2011), Alamin Somo na Ahmed Hussein (*Shangwe ya Ushairi* 2011) Alamin Mazrui (1988) ambaye ndiye mshairi wa pwani alifanya majaribio na kuandika diwani ya mashairi huru. Baadhi ya washairi hawa walianza kutunga kwa kuchapishiwa mashairi yao katika magazeti.

Ahmad M. Msallam katika kitabu chake *Chozi la Damu* (2009) ni mkusanyiko wa insha ambamo maudhui yaliyotolewa kwa ufasaha. Katika kila insha, mwandishi ambaye pia ni mtunzi wa mashairi, ametunga shairi au mashairi ya kutilia mkazo na kufafanulia mada yake. Mohamed Khamis Hemed (2017) ni mshairi mwingine aliyetunga diwani ya *Tele Haitunguliwi*. Mshairi huyu pia ana mashairi mengi yanayosambaa kwa njia ya majukwaa ya kulikoni na njia nyingine za mitandao.

Kuna na wengine ambaao ni washairi watajika lakini kazi zao hazijapishwa katika vitabu. Hawa ni washairi kama Sheikh Seif bin Akida bin Ahmad al Mauly (Vanga) aliyejewa mshairi na pia alikusanya mashairi mengi ya Kivumba, Kipemba na ya Kimrima, Sheikh Hemed bin Abdalla (Majambo), Sheikh Muhammad bin Mshihiri (Asad – Wasini) aliyejewa mshairi wa Kivumba. Maalim Sayyid Abdurahman Saggaf Alwy, Sheikh Mohamed Famau Shalii (Malindi) ambaye kulingana na Mau alikuwa mshairi hodari. Faraji Bwana Mkuu, Sheikh Abdallah BaKathir ‘Kadara’ na Rehema Faruqi (hawa watatu walikuwa walimu wa Ahmed Sheikh Nabahany wa kutoka Lamu na Pate ) na Mahmoud Abdulkadir (Mau). Kulingana na Chiraghdi (1971) katika utangulizi wa *Malenga wa Mvita* anasema kuwa ngano na mashairi mengi yamepotea au tarehe zake hazijulikani kwa sababu ni mapokezi tu na yamepokezwa kwa maneno na sio kwa njia ya maandishi.

Mbali na hawa kuna wale washairi wengi wanaotunga na mashairi yao yanapatikana katika gazeti la Taifa Leo. Hawa ni kama vile Abdalla Shamte, Mahmoud Hassan Barroh, Mohamed Shaban Ali, Juma Ali Shumbana, Awadh Basheikh, Tyson Ty Belle Katana, Soudy Podos na wengi wengine.

### **Washairi wa Kiume kutoka Bara**

Ijapokuwa hawa walianza kutunga katika miaka ya baada ya Uhuru, hivi leo kuna washairi kadhaa wa kutajika wanaoangukia katika tapo hili na kuna wengi zaidi ambaao wanatunga mashairi. Baadhi ya hawa walianza kujilingiza katika uwanja wa mashairi katika magazeti ya Kiswahili humu nchini. Walijilingiza kwenye magazeti kama Taifa, Mseto, Chemsha Bongo na Kenya Leo (tazama Wallah 1988). Mtunzi kama Wallah bin Wallah ana diwani (*Diwani ya Ziwa Kuu* (ziwa la Nyanza) ambayo ndani yake anakiri kuwa:

Natumaini hadi muhula huu, hiki ndicho kitabu cha pekee cha kipekee cha mashairi kilichoandikwa na mwenyeji mzaliwa wa pande hizi za ziwani. Mtakubaliana nami kwamba masikio yetu yamejaa mawimbi ya majina ya washairi kutoka mabonde ya ufukwe wa bahari kuu (Hindi). Aidha macho yetu yamepata kiwi kwa kutizama na kuona vitabu (hasa diwani) vilivyopambwa kwa majina yayo hayo ya kimwambao (1988: xii).

Walibora (2007: xi-xii) naye anasema:

ni muhimu kutambua kuwa enzi ya ushairi wa Kiswahili kuwa miliki ya Waswahili asilia imepita ... Kwa maneno mengine, watu wa asili mbalimbali wameivulia bahari ya utunzi wa mashairi kwa kutumia Kiswahili kama nyenzo ya kubebia hisia zao, mihemko na mawazo yao.

Mshairi ambaye tunaweza kusema ametunga kwa mapana ni Kithaka wa Mberia. Wa Mberia (keshatajwa) ana vitabu kadhaa vya mashairi. Miongoni mwa vitabu vyake vya mashairi ni kama vile: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Msimu wa Tisa* (2007), *Rangi ya Anga* (2014), *Redio na Mwezi* (2005) na *Doa* (2018)). Mshairi mwingine wa bara ni Kineene wa Mutiso mwenye diwani, *Mizani Yangu*. K. W. Wamitila amekusanya na kuhariri tungo zake na za watunzi kadhaa wakiwemo wa bara kama Timothy Arege, Kineene wa Mutiso na Nyambari Nyangwine (mashairi mawili) katika *Tamthilia ya Maisha* (2005). Pia, ana kazi nyingine ambapo tunapata tungo zake pekee (*Kaza Macho*,

2014). Timothy Arege (*Tunu ya Ushairi* 2013) naye amehariri diwani ambayo ndani yake kuna mashairi yake na washairi wengine watatu mmoja kutoka Tanzania na wawili wakiwa kutoka pwani ya Kenya.

Walibora (2007) amehariri diwani ambayo ina washairi kadhaa wa bara na wa pwani. Kwa mfano, ye ye mwenyewe amehariri diwani iliyowahusisha, Wamitila, Kineene wa Mutiso, Omar Babu, Muchai bin Chui, Paul Nabiswa na Timothy Arege kati ya wengine (Douglas Mutua na Hezron Mugambi). Pia, amehariri diwani ya *Waja Leo* ambayo imekusanya mashairi ya washairi kumi na wawili. Baadhi ya washairi ndio kazi zao za mwanzo kuchapishwa katika kitabu na kama asemavyo Walibora (2007), kati ya mafundi wa kulumbana “kuna walumbi, pamoja na watanzi wa mashairi wa daraja mbalimbali tokea malumbukeni, chipukizi, washairi, malenga na hata maustadh.” Diwani nyingine ni *Miali ya Ushairi* iliyokusanya na Iribi Mwangi na Wamalwa (2016) ambayo kuna mashairi ya watanzi mbalimbali. Kwa mfano, tunapata mashairi yao wenye na wengine kama Wendo Nabea, Omar Babu, Kirimi Mitambo, Kitula Kin’gei na mengine kutoka vitabu ambavyo vilichapishwa kitambo. Omar Suleiman (Mzee Pembe- Kiroboto) naye ana mkusanyiko kwa jina Sheikh Samragaat Miraa.

Katika kundi hili pia tunapata washairi wengi wanaoandika katika Taifa Leo, Jumapili na Jumatatu kwenye ukumbi wa Sokomoko. Mifano ya washairi hawa ni Mukoya Aywah, Hosea Namachanja, Peter Wanjohi, Boaz Aseli, Moses Chesire na Abdala Savange mionganoni mwa wengine. La muhimu ni kuwa hawa ni watanzi wa kutoka makabila mbalimbali ya Kenya.

#### **Washairi Wanawake: Kutoka Pwani na Bara**

Inasemekana kuwa kumekuwa na washairi kadhaa wanawake ambao baadhi yao hata waliwaathiri baadhi ya washairi wa kiume. Washairi hawa wanaume waliathiriwa au walikitwa na washairi wa kike katika familia zao. Kwa mfano, mamake Mahmoud Abdulkadir inasemekana alikuwa mtungaji mashairi (Timammy (2013-14), Frankael na Mau (2013). Pia, nyanyake Nabahany aliyeleka alikuwa mshairi (Mulokozi na Sengo 1995). Hata hivyo, ni kazi chache sana zilizopatikana ambazo zinaweza kusema ni za watanzi hao wanawake. Kazi maarufu sana iliyopo ni ya *Utenzi wa MwanaKupona* ya Mwana Kupona Binti Mshamu ulioandikwa 1854. Naye Amina Abubakar Sheikh (1880- 1975) ndiye mshairi aliyetajika wakati wa kipindi cha ukoloni. Alizaliwa Pate na kuishi Lamu. Aliandika mashairi kuhusu matatizo ya maisha, dini na mahusiano ya watu na inasemekana mengi ya mashairi haya yamepotea. Rukiya Muhammad al Busaidy (1882-1968) ni mshairi mwengine wa Lamu aliyetunga mashairi, na tunaambiwa na Shariff (1988: 57) kuwa alitunga kwa mtindo wa Tiyani Fatiha ambao sijapata kuuona katika kazi nyingine zozote. Ijapokuwa tunaangalia washairi wanawake wa Kenya, hatuna budi kumtaja mshairi maarufu wa Zanzibar, Zaynab Himid aliyeandika mashairi mengi na tenzi mbili maarufu ‘Howani Mwana Howani’ na ‘Mwana Kukua.’

Washairi wengine ni Khadija Abdulhussein aliyeleka mke wa Ahmed Sheikh Nabahany na Zena Mahmoud ambaye ni mtoto wa Rukiya Muhammad. Zena Mahmoud alikuwa ametunga kazi za kishairi na kazi nyingine ambazo ni za kidini alizozitafsiri kwa ushairi kama tawasuli kwa Kiswahili. Wapo washairi wengine wanawake lakini hawajachapishwa kabisa kwani kazi zao nyingi ni kazi ambazo wanatunga na kughaniwa katika shughuli mbalimbali za kijamii na hupitishwa kwa njia ya mdomo na hapa ndipo tunapopata wanawake wengi wa pwani. Mifano ya washairi hawa ni kama Zaharia bint Maimun na Swabra Sheikh (Lamu). Hawa, kwa kawaida, huombwa na wanajamii wawatungie mashairi kuakisi mambo tofauti yanayotendeka. Mfano wa wa matukio au shughuli mbalimbali zilizotungiwa mashairi ni kama zile za arusi zilizohusisha kupeleka begi, kupokea bwana harusi na kupamba. Nyingine zilihusisha kutoa wasia kwa maarusi na kuwatahadharisha kuhusu maisha ya ndoa, kuliwaza waliofiwa, kuaga wanaokwenda Maka na kadhalika. Wengine huwatungia waimbaji wa taarab kwa mfano Khulaita Mohamed Said alikuwa akimtungia Malika au mwimbaji mwengine aitwaye ‘Jugnu’ na Amira Mselem Said (Mombasa).

Katika utafiti wetu, tulipata wanawake wachache sana wanaoandika katika gazeti la Taifa leo. Kati ya kipindi cha baina Agosti 2018 na Mei 2019 tumejapata tu wanawake wawili wakichangia shairi mojamoja. Hawa ni Zuhura Mzee na Mwanaidi binti Salimu Zani.

Kwa hakika, ni washairi wachache sana wanawake wa bara ambao wamechapishwa. Katika Diwani ya *Waja Leo* (2012) tunawapata washairi Emily Ondeko, Pauline Kea na Anne Samba ambao kila mmoja amechangia mashairi mawilimawili. Hata hivyo, mionganoni mwa mashairi hayo, mashairi matano ni mashairi huru na shairi moja la Pauline Kea ndilo shairi la kiarudhi. Kati ya kipindi cha Agosti 2018 na Mei 2019, tumejapata washairi wanne waliochapisha mashairi katika gazeti la Taifa leo. Hawa ni Sophy Onura akiwa na shairi moja, Grace Shako Marura shairi moja, Loice Anet Nasimiyu shairi moja na Martha Gaceri mashairi matatu.

### **Maudhui ya Mashairi**

Amana (1982: vii) anadai kwamba “kama ilivyo kawaida ya watunzi, tungo zao hutokana na mwamko wa tukio, kisa ama hisia fulani.” Hili, kwa hakika, ni kweli kwa washairi wote wa pwani na bara ijapokuwa zipo tofauti za kimaudhui ambazo zinaweza kuwatofautisha. Falsafa au dhana kuwa dunia siyo makao yetu ya kudumu, pamoja na falsafa kuhusu umasikini na ya mtu kuridhika na alichochi nacho, ni mionganoni mwa mambo yanayozungumziwa na washairi hawa wa pwani. Haya hasa yanatokana mafunzo ya dini ya Kiislamu na ndio tofauti kuu kati ya washairi wa pwani na bara. Maudhui mengine muhimu yanayoandikiwa na washairi wa pwani ni utu, busara na tabia njema, majisifu, maisha, mapenzi, ubaya wa ubaguzi na siasa. Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba wanazungumzia masuala ya mawaidha kwa mapana. Tuikitaoa mifano ya watunzi tofauti, kwa mfano tukimrejelea Fumo Liyongo, Liyongo alikuwa na nyimbo kadhaa za aina ya utumbuizo na utendi wa Mwana Manga uliomsifu Mwana Manga. Huu ulisifia uzuri wa Mwana Manga. Pia, kuna na utumbuizo wa mnazi ambao ni nyimbo ya sifa.

*Utenzi wa Mwana Kupona* unajulikana sana kwa mawaidha kwa mabinti ndipo El Maawy (2011) alifikiria jawabu ya Mwana Kupona ili faida imfikie mke wa kileo. Utunzi huu ni njia ya kuzindua na kuyadumisha maisha ya kinyumbani na mtunzi amejifanya mwanamke na kumjibu Mwana Kupona kulingana na maisha ya wakati huu wa kisasa. Hapa chini ni mfano wa ubeti wa Mwana Kupona na jawabu la ubeti huo.

Sitangane na watumwa	Yapisile wangu mama
Ila mwida wa huduma	hakuna tena utumwa
Watakuvutia tama	kutangamana lazima
Labuda nimekwambia	usawa ukitimia

Kwa hakika, maudhui ni mengi kama vile walivyo washairi wa kila kikundi wa pwani na bara. Mashairi ya bara zaidi hushughulikia mambo yanayowashughulisha au yanayowagusa (maswala ibuka) kwa mfano, wanaandikia siasa na uongozi na kuhakiki mifumo ya kileo kwa kuangalia ubora wake na udhaifu. Masuala mengine ni mageuzi, nasaha, mazingira, unafiki, ubinafsi, utaifa, mapenzi, msako wa nafsi, mauti na falsafa kuhusu maisha. Kwa hivyo, katika makala yetu tutamchukua mshairi mmoja kutoka kila kundi tuonyeshe maudhui aliyoshughulikia.

Kulingana na Chiraghdin (1971) katika utangulizi wa *Malenga wa Mvita* (1971), anasema kuwa “mashairi ya Kiswahili yametanda katika mambo yote yanayomhusu binadamu, mazingira yake, fikra na mawazo yake.” Kwa mfano, Ahmed Nassir ametunga kueleza hali ya dunia na binadamu walivyo au mambo ya kilimwengu. Ametunga kuhusu mapenzi, machukivu, maonevu, misiba na maliwazo, mzaha na unyumba. Pia, ametunga mashairi ya kujigamba, kusuta na kukejeli. Anayo pia mashairi ya kuonyesha umbuji wake wa lugha au kueleza matumizi mbalimbali ya neno kwa kulitungia shairi hilo.

Kwa upande wa mashairi ya Kithaka wa Mberia, tunaona kuwa maudhui yake yanaweza kuangukia katika maeneo matatu. Kuna maudhui ya siasa ambapo anazungumzia uongozi mbaya katika bara la Afrika, udikteta, ukandamizaji /unyanyasaji na dhuluma za ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Kuna yale yanayozungumzia kuhusu uharibifu wa mazingira na rasilimali za

kiasili, kwa mfano shairi la “jinamizi” (*Bara Jingine*). Katika shairi hili anazungumzia masuala anuai kuhusiana na ekolojia anapoangazia mtagusano kati ya jamii na ekolojia. Ameonyesha jinsi wanajamii wanavyoathirika wanapoharibu rasilimali za kiasili kama vile misitu, mito na mabwawa, pia hali ya anga na ardhi, na jinsi swala hili linavyoweza kurekebishwa. Eneo la tatu analogzungumzia mwandishi huyu linahusiana na masuala ya kijamii kama vile ubaguzi wa kijinsia. Hapa anazungumzia maswala kama vile dhuluma za kimpenzi, kunyanyaswa kwa wasichana kielimu, tamaduni zilizopitwa na wakati kama ukeketaji wa wasichana, ndoa za mapema za wasichana au kuwaoza kwa wazee na dhuluma za kinyumbani. Maudhui mengine ni matumizi na athari za dawa za kulevyta, UKIMWI na athari zake, uzinzi pamoja na uasherati (*Rangi ya Anga* 2014). Mshairi Omar Suleiman ambaye ni wa bara lakini Muislamu ametunga mashairi mengi kuzungumzia kuhusu miraa au khaat na athari zake. Pia, mashairi yake mengine yamejikita katika kuusia juu ya mambo ya ulimwengu au kuhusu mambo yanayowapata binadamu katika maisha yao.

Tofauti nyingine kwa upande wa maudhui, ni kuwa katika tungo za pwani kuna kazi nyingi zilizotungwa za kidini au zenyé maudhui ya kidini. Kwa kuwa watunzi wengi wa pwani ni Waislamu hawakuweza kuepuka swala la dini. Hata pale wanapotunga kuhusu maudhui yasiyokuwa ya kidini, bado huyapa mtazamo wa kidini. Wakati huo, licha ya mashairi ya bara kutungwa na washairi amba ni Wakristo, hakuna mashairi au tungo zinazozungumzia dini ya Kikristo. Tunampata hata mshairi Somo akitoa onyo kwa yejote atakayezitumia tungo zake kinyume na sheria ya dini ya Kiislamu na kuwa ataenda kumdati mbele ya Mungu kesho akhera. Wale washairi wa bara amba ni Waislamu, huwa wameathiriwa na dini katika utenzi wao. Mfano wa tungo zinazozungumzia dini ya Kikristo ni tungo za Mathias Mnyampala kutoka Tanzania ambaye ana utenzi wa “Enjili takatifu” na utenzi wa “Zaburi.”

### Mitindo

Tofauti ya kwanza muhimu ni kuwa katika maeneo ya pwani kuna ushairi simulizi mwangi sana amba huishia kupotea au beti zake chache kuhifadhiwa akilini kwa vile mara nyingi ushairi huu hutungwa papo kwa hapo au huwasilishwa kutohaka na kumbukizi ya mwasilishaji wake. Au pengine hubakia katika karatasi zilizoandikiwa hali katika sehemu za bara hakuna ushairi simulizi mwangi pengine ule unaotungwa kwenda kughaniwa katika mashindano ya kitaifa ya shule ya ukariri wa mashairi (tungo ambazo zimeandikwa kwa minajili ya kuwasilishwa mbele ya hadhira).

Tofauti nyingine kuu kati ya washairi wa pwani na bara ni kuwa mara nyingi watunzi wa pwani wanapoandika wanatumia lugha zao za kwanza ambazo ndizo lahaja za Kiswahili ndipo tunamuona Hussein (2011) hata akisema,

Takuenzi Kimvita, ndimi za wangu wavyazi  
Tangu n’lipovuwata, nkivuata maozi  
Ndiposa hakimbata, kana sindano na uzi  
Ndimi yangu taienzi, hatukuza kimvita

Kwa washairi wa Mvita au Mombasa tokea enzi za kina Muyaka, Abdilatif Abdalla, Ahmad Nassir, Alamin Somo na wengine, hii ndio lugha walitumia. Washairi wengine wa pwani wametunga kwa Kiamu. Washairi hawani kama vile Muhammad Kijumwa, Zena Mahmoud, Ahmed Msellel na Mahmoud Abdulkadir na wengineo. Tunapata wengine wakitunga kwa Kivumba, kwa mfano Boukhet Amana na Hassan Mwalimu Mbega. Washairi wengine walitunga kwa lahaja ya Kimrima. Washairi wa bara hujaribu kutumia maneno ya kilahaja lakini ni lazima wafanye utafiti kuyaewela hayo maneno na jinsi yanavyoendelezwa. Kwa mfano, Iribemwangi (2016: 95) katika shairi ‘lipi la kuchagua’ anatumia neno mutuzi badili ya mtuzi. Mbali na kuwa washairi hawa walitumia lahaja zao, wengi wao katika baadhi ya mashairi yao hutumia lugha ya kale na ngumu zaidi ya ile inayotumiwa na wengi wa washairi wa bara ambayo huwa ni ya kawaada zaidi. Mifano ya washairi hawa ni kama Muyaka, Ahmad Sheikh Nabahany, Ahmad Nassir na wengineo. Kulingana na Habwe (2017: iii) katika utangulizi anasema kuwa

mshairi wa Tele Haitunguliwi amejitahidi katika kuingia katika tasnia ya ushairi. Unaposoma mashairi yake unaona amedhibiti lugha na hata ufundi wa kimapokeo wa vina na mizani.....lugha yake ni ya satua ya juu.

Tofauti nyingine ipo katika utungaji wa tenzi. Huu ni muundo uliopendelewa sana zamani na ambao ulitumika kujadilia maswala yanayohitaji kina katika kuyaelezea mathalani maswala ya kidini na kuwa idhi. Tenzi nyingi sana zimetungwa na washairi wa pwani na ni watunzi wachache sana wa bara waliojaribu kutunga tenzi. Kwa mfano tukichukua mtunzi kama Mahmoud Abdulkadir wa Lamu ana tenzi nyingi sana kwa mfano Wasiya wa Banati (1974), Kimondo (1975), Ukimwi ni Zimwi (1990), Haki Haizami (2000), Uzinduzi (2001), Mwongozo (2002), Mukhadharati (2004), Ramani ya maisha ya ndowa mume (2006), Ramani ya maisha ya ndowa mke (2006), Kikuba (2010) na Wema (2017). Tenzi nyingine ni kama Utensi wa Adamu na Hawaa wa Abdilatif Abdalla, utenzi wa Mtu ni Utu na wa Irshadi za Ahmad Nassir na nyengine nyingi za awali na za karibuni. Kwa washairi wa bara, Wamitila (2014) ana utenzi wa ‘ndovu na mja’ ijapokuwa si mrefu sana kama tenzi nyingine una beti 75. Na ijapokuwa unaanza na formula za kuanzia tenzi kwa mfano kuitisha kalamu na karatasi lakini anaepuka kutanguliza kwa kumuomba Mungu na kumuombea mtume na maswahaba kama ilivyo kaida ya kuanzia tenzi zilizoandikwa na washairi Waislamu.

Muundo mwengine uliokuja kupendelewa baadaye ni muundo wa tarbia. Chambilecho Mazrui (1988),

Katika historia ya fasihi ya Kiswahili, tanzu ya mashairi mpaka hivi karibuni ndiyo imeshika bendera ikajaa katika nyoyo za Waswahili na kupanya na kusambaa katika maisha yao mpaka tanzu zingine zozote zikafifia.

Hili kwa kiasi fulani ni kweli, ijapokuwa kuna washairi wabunifu wakiubadilisha mtindo huu wa tarbia. Kwa mfano Amana (1982) ametunga akitumia bahari ya msuko ambayo ni ufupisho wa maneno ya kibwagizo katika shairi ‘wasia sikiza’ (uk. 38) na ‘siwe’ (uk. 83) Pia Abdilatif (1971) ana mashairi yenyne kibwagizo kifupi. Amana ametunga akitumia ukumi katika shairi ‘narun hamia’ (uk. 46). Washairi wa pwani walianza kuibadilisha ile mitindo ya awali. Lakini washairi wa bara wameibadilisha zaidi kwa sababu ni wasomi na waliathirika na kazi walizoziona kutokana na usomi huo. Tunaona wakitunga mashairi yenyne mishororo yenyne vipande viwili, vitatu au zaidi, kuwa na kibwagizo kuwa katika mshororo wa kwanza au katikati ya ubeti na kadhalika. Chambilecho Arege (2013: vii)

Kuhusiana na mpangilio wa mistari katika mashairi ya Diwani hii, yapo mashairi yenyne mstari mmoja katika kila ubeti hadi ya mistari kumi kila ubeti. Kuna hata shairi lenye mistari kumi na mine kila ubeti, ... .Kwa upande wa mpangilio wa maneno kuna mikondo mingi ya bahari ya pindu.... Bahari ya kikwamba nayo imechukua mikondo mbalimbali....Upo vilevile upya wa vibwagizo.....

Kuna na tofauti ya kuwa washairi karibu wote wa pwani wanatunga wakifuata arudhi za ushairi wa Kiswahili isipokuwa Abdilatif ana shairi ‘kibaruwa’ na Alamin Mazrui ana mkusanyiko wa mashairi huru- *Chembe cha Moyo* (1988). Mazrui anakiri kuwa:

muundo wa mashairi mengi yaliyomo katika mkusanyiko huu umetoka katika mipaka ya ule muundo tuliozoea na tulioupokea kutoka kwa wahenga wetu kwa kuwa haufuati kanuni za arudhi yaani kanuni za vina, vituo na mizani” (uk. vii).

Washairi wa bara wengine pia hutunga mashairi ya arudhi, hasa wale wanaochapisha katika Taifa Leo. Wote hawa hutunga wakitumia arudhi na hata wengine waliochapisha diwani ijapokuwa tofauti ni kuwa kwa baadhi ya washairi hawa wa bara maswala ya vina na mizani ni kama inaonekana yanalazimishwa. Miongoni mwa wale wa pwani, inaonekana vina na mizani vinakuja kwa urahisi pengine kutokana na tajriba yao ya lugha. Kwa vile wengi wanaoandika miongoni mwa washairi wa pwani ni wale wenye kipawa na tajriba katika taaluma ya ushairi. Hali hii ni tofauti na ya washairi wa bara ambao wengi wao wamejifunza kutunga na wengine huwa hawajaijua lugha na unapoangalia mashairi yao unakuta misamiati ikirejelewa.

Mashairi huru yanatungwa tu na washairi wa bara. Kithaka wa Mberia, kwa mfano, ana mikusanyiko au vitabu sita vya mashairi huru. Wengine waliotunga mashairi huru ni watanzi kama Wamitila, Kineene wa Mutiso na Arege mionganoni mwa wengine.

Katika ushairi huu huru, baadhi ya washairi wa bara pia hutunga mashairi ya mchoro au mashairi picha. Kithaka wa Mberia ana mashairi kama ‘boga’ (uk.2), ‘nyumba’ ( uk.17), ‘dau haliendi’ (uk.32) katika *Mchezo wa Karata*. Pia, ana mashairi kama ‘mruko wa nyuki’ (uk.20) na ‘mwashi mahiri’ (uk.45) katika *Bara Jingine*. Wamitila naye anayo mashairi ya mchoro kama shairi la ‘paukwa pakawa’ (uk.78) katika *Tamthilia ya Maisha* ambalo lina picha ya ramani ya bara la Afrika. Pia kuna shairi la ‘iweje’ (uk.7) linalotoa picha ya alama ya kiulizio na ‘duaran’i (uk. 52) katika *Kaza Macho*. Naye Arege anayo mashairi ya mchoro kama ‘vidato vya maisha’ (uk.59) au shairi la ‘maisha vidato’ la Joseph Kiponda (uk.159) katika *Tunu ya Ushairi*. Picha hizi zimetumiwa kuakisi maudhui mbalimbali.

Swala lengine ambalo kuna tofauti kati ya washairi wa pwani na bara ni katika uchapishaji. Washairi wa bara wamechapishiwa au wengi wamejichapishia kazi zao wenyele ilhali washairi wa pwani si wengi waliochapishiwa kutokea miaka ya tisini na kuna wachache amba wamejichapishia kama Basaidah (2011) na Somo (2011, 2012, 2017). Pengine sababu ni kuwa washairi hawa wa bara ni wasomi na wana uwezo wa kujitafutia wachapishaji wakitarajia kuuza vitabu vyao hali washairi wa pwani hawatilii maanani sana kuchapishwa kwani kwao zaidi ni haja yao kupitisha ujumbe na swala la kufaidika si muhimu sana pengine kutokana na dini kuwa wanaamini kila neema Mwenyezi mungu aliowapa wataulizwa. Kuna washairi wengi wanaowatungia watu mashairi kuakisi shughuli zao mbalimbali maishani mwao bila ya kupatiwa malipo yoyote.

### **Mapendelezo**

Baada ya kuangalia kwa jumla, tumeweza kubaini kuwa kuna ushairi mwangi amba siku hizi unapitishwa kupidia vyombo vya habari kama magazeti kwa mfano gazeti la Kiswahili la Kenya – Taifa Leo, ambalo huchapisha ukurasa mzima wa mashairi kila siku ya Jumatatu na ambayo yote huwa ni mashairi ya arudhi. Kuna pia mashairi yanayopatikana kwa njia mpya za teknolojia kwa mfano majukwaa ya kulikoni na twita, instagramu na mengineyo. Wakati wa kipindi cha uchaguzi nchini Kenya katika sehemu za Lamu kulikuwa na mashairi mengi ambayo yalikuwa yakipitishwa kwa njia ya simu za mkononi ambayo baada ya kipindi hicho yalipotea. Isisahauliwe katika matini hii tumeangalia zaidi watanzi amba wamepata kuchapishwa hali tunajua kuwa mashairi mengi yanatolewa kwa njia ya kutongolewa au kughaniwa hadharani katika shughuli mbalimbali ijapokuwa hili zaidi hutokea pwani. Kama asemavyo El Maawy na Alawy (2011: xii)

Waswahili walikuwa na kale yao, ambayo yaonekana katika mashairi yao ya zamani kwa sababu mashairi ndiyo yaliendelea kwa dahari, yakadumu na kutufikia mpaka sisi. Waandishi na wachunguzi waliotaka kujua mila za Waswahili na maisha yao yalivyokuwa waliweza kuyapata zaidi haya kutokana na ushairi wao kutokana na mengineyo.

Kuna nyanja nyingine ambayo haikutajwa kabisa pia ambayo ni ushairi wa kasida. Hizi ni tungo za kidini ambazo hutungwa kila uchao na walimu/maustadh au maustadha wa vyuo na madrassa mbalimbali nchini kote Kenya. Hivyo, huu ni uwanja mpana amba unahitaji kutafitiwa kwa kina. Kuna pia mashairi yanayosikika katika idhaa mbalimbali ambayo mengi yake huwa ni ya arudhi ambayo pia yanahitaji kukusanya.

### **Hitimisho**

Katika makala haya tumeangalia kwa jumla sana ushairi wa Kiswahili wa pwani na bara wa Kenya. Lengo hasa ni kuonyesha upana wa taaluma hii na jinsi ambavyo kuna washairi wengi na ushairi mwangi sana amba haujatafitiwa. Tumeonyesha kwa kijumla maswala ya kimaudhui yanayoshughulikiwa na washairi hawa na pia tofauti za kimtindo kati ya ushairi wa pwani na bara. Kama ambavyo tumetaja kuna mashairi mengi ambayo hayajkusanya na kuchapishwa na hili hasa linatokana na kuwa ushairi unapuuzwa. Kule ambako unatiliwa maanani au kupewa kipau mbele

yaani sehemu za pwani huwa ni ushairi simulizi ambao huwa unatumika na kubakia akilini au katika miswaada. Hivyo, tunawahimiza wataalamu mbalimbali wajitokeze kuufanya utafiti ushairi huu.

### **Marejleo**

- Abdalla, A. (1973). *Santi ya Dhiki*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Oxford University Press.
- Abdulkadir, M. A. & Frankl, P. J. L. (2013). ‘Kiswahili’: A poem by Mahmoud Ahmad Abdulkadir to which is appended a list of the poet’s compositions in verse. Swahili Forum 20: Pg 1-18.
- Abedi, K. A. (1973). *Sheria za Kutunga Mashairi na Divani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Alawy, A. S. na El-Maawy A. A. (2011). *Kale ya Washairi wa Pemba Kamange na Sarahani*. 1<sup>st</sup> Edition. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Oxford University Press.
- Arege, T. (2013). *Tunu ya Ushairi*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Oxford University Press East Africa.
- Basaidah, T. A. S. (2011). *Bustani ya Mashairi*.
- Chiraghdin, S. (1971). ‘Utangulizi wa Mhariri’ Kwenye Nassir A. *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford 1971.
- El-Maawy, H.S. (2009). *Waswahili na Utamaduni Wao*. 1<sup>st</sup> Edition. Lamu, Kenya.
- El-Maawy, A. A. (2011). *Jawabu la MwanaKupona*. 1<sup>st</sup> Edition. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Habwe J. (2017). ‘Utangulizi kwenye Mohamed K.H. Tele Haitunguliwi’. Nairobi Frelis Windows.
- Harries L. (1967). *Utenzi wa Mkunumbi*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Iribemwangi P. I. na Wamalwa, K. (2016). *Miali ya Ushairi*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Karama S. (1985). *Nyota ya Ushairi*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Heinemann.
- Karama S. na Khan, M. (1973). *Kusoma na Kufahamu Mashairi*, Kitabu cha 1. 2<sup>nd</sup> Edition. Nairobi: Longman Kenya Limited.
- Karama, S. na Khan, M. (1974). *Kusoma na Kufahamu Mashairi*, Kitabu cha 2. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Longman Kenya Limited.
- Kezilahabi, E. (1973). ‘The Development of Swahili Poetry: 18<sup>th</sup> Century to the present’. *Kiswahili*. Vol 42/2,43/1, Dar es Salaam: TUKI.
- Khamis, H. M. (2017). *Tele Haitungulini*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Frelis Windows.
- Knappert, J. (1979). Four Centuries of Swahili Verse, A Literary History and Anthology. 1<sup>st</sup> Edition. London: Heinemann Educational Books Limited.
- Mazrui A. (1988). *Chembe cha Moyo*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Mbega, H. M. (1986). *Dafina ya Umalenga*. 3<sup>rd</sup> Edition. Nairobi: Longman Kenya.
- Mbega, H. M. (1975). *Upisho wa Malenga*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Mberia, K. (1997). *Mcbezø wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications.
- Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications.
- Mberia, K. (2014). *Rangi ya Anga*. Nairobi: Marimba Publications.
- Mberia, K. (2007). *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publications.
- Mberia, K. (2005). *Redio na Mwezi*. Nairobi: Marimba Publications
- Msallam, A. M. (2009). *Chozi la Damu*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Communicart Limited.
- Mulokozi, M. na Sengo, T. (1995). *History of Kiswahili Poetry A.D. 1000-2000*. 1<sup>st</sup> Edition. Dar es Salaam: TUKI.
- Mzenga, M. na Hijazy, S. O. (1977). *Tujifunze Mashairi*. 1<sup>st</sup> Edition. HongKong: Macmillan Education
- Nabhany, A. S. (2011). *Mapisi ya Waswahili na Lugha yao ya Kiswahili*. 1<sup>st</sup> Edition. Dar es Salaam: Aera Kiswahili Researched Products.
- Nassir, A. (1982). *Taa ya Umalenga*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Nassir, A. (1971). *Malenga wa Mvita, Divani ya Ustadh Bhalo*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Oxford University Press Limited.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasibi Nadharia na Mbinu*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. 1<sup>st</sup> Edition. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. 1<sup>st</sup> Edition. Eldoret: Moi University Press.

- Suleiman, O. (1973). *Sheikh Samragaat Miraad, Kitabu cha Mairongi*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Foundation Books.
- Somo, A. & Hussein, A. (2011). *Sauti ya Shangwe*. 1<sup>st</sup> Edition. Mombasa.
- Somo, A. (2017). Biladi. Mombasa Shekha Enterprises.
- Timammy, R. (2014). Shaykh Mahmoud Abdulkadir ‘Mau’ (b.1950): A reformist Preacher in Lamu. The annual Review of Islam in Africa. Issue no.1211 2013-14.Pg 85-90.
- Walibora, K. (2007). *Dinani ya Karne Mpya*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Phoenix.
- Walibora, K. (2012). *Waja Leo*. Nairobi Oxford.
- Wallah bin W. (1988). *Malenga wa Ziwa Kuu*. 8<sup>th</sup> Edition. Nairobi: East African Educational Publishers
- Wamitila, K. W. (2005). *Tamthilia ya Maisha*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Wamitila, K.W. (2014) *Kaza Macho*. 1<sup>st</sup> Edition. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.